


EPISCOPAL CHURCH of the
HEAVENLY REST

God's Love. For All.

Jumapili ya Nne ya Pasaka
Sala ya Asubuhi
Jumapili, Mei II, 2025
Saa 1:00 jioni



The Fourth Sunday of Easter
Morning Prayer in Swahili
Sunday, May II, 2025
1:00 in the afternoon

SHAIRI LA SIKU

Yesu alisema: Kondoo zangu wnasikia sauti yangu, nami ninawapa uzima wa milele.

Yohana 10:27, 28

WIMBO WA KUINGILIA

Wote kusimama

WITO WA KUABUDU

Tumekusanyika pamoja kama jamaa ya Mungu mbele ya Baba yetu, tukivutwa na Roho yake, kusifu Jina lake, kusikia na kupokea Neno lake takatifu. kumwomba usamehe kwa zambi zetu, kuombea mahitaji yetu na ya dunia, kufurahi katika mapendo yake, na kutumwa katika salama yake.

MWALIKO

Ee Bwana, ufungue midomo yetu.

Na kinywa chetu kitaonyesha sifa yako.

Katika KUZALIWA, ONYESHO, na PASAKA:

Matendo ya Bwana ni makubwa na ya ajabu!

Wakati tulikuwa tungali katika giza, alisikia kilio chetu.

Mapendo ya Mungu yameonekana kwetu.

Alituma Mwana wake ili tupate uzima wa milele.

Wimbo wa Biblia au wimbo mwingine.

WIMBO

KUUNGAMA DHAMBI

Muhudumu aseme:

Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli si ndani yetu.

Tukikiri zambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, hata atatuondolea zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote.

I Yohana 1:8-9

Muhudumu aseme:

Tukiri zambi zetu kwa Mungu Mwenyezi.

Wote wapige magoti na kusema

Mungu Mwenyezi, Baba yetu ya mbinguni, tumekosea wewe, na tumekosea jirani zetu, kwa mawazo yetu, na kwa maneno yetu, na kwa matendo yetu, na kwa maovu tuliyoyatenda, na kwa mema tusiyoyatenda, kosa letu wenyewe. Sisi tunatubu kabisa. Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo, utusamehe yote yaliyopita; utuwezeshe tangu leo kukutumikia, katika upya wa uzima. Kwa utukufu wa Jina lako. Amina.

Muhudumu au mutu mwengine asiye Kasisi, akipiga magoti atumie ombi hili.

Ee Mungu, mwenye rehema, tunakusihi, utupe sisi, watu wako waaminifu, usamehe na salama, ili tusafishwe zambi zetu zote, na tukutumikie na nia tulivu; kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

Wote **Amina.**

OPENING SENTENCE

Jesus said: My sheep hear my voice, and I give them eternal life.

John 10:27, 28

PROCESSIONAL HYMN

Stand for the Procession

CALL TO WORSHIP

We are gathered together as God's family before our Father, drawn by his Spirit, to praise his Name, to hear and receive his holy Word. to ask him to forgive us for our sins, to pray for our needs and the needs of the world, to rejoice in his love, and to be sent to his safety.

INVITATORY

O Lord, open our lips.

And our mouth shall proclaim your praise.

At CHRISTMAS, EPIPHANY and EASTER:

The works of the Lord are great and wonderful!

While we were still in the dark, he heard our cry.

God's love has been revealed to us.

He sent his Son so that we may have eternal life.

A song from the Bible or another song is sung.

HYMN

CONFESSION OF SIN

The Minister should say:

If we say that we have no sin, we deceive ourselves, and the truth is not in us. If we confess our sins, he who is faithful and just will forgive us our sins and cleanse us from all unrighteousness.

1 John 1:8-9

The Minister should say:

Let us confess our sins to God Almighty.

All should kneel and say:

Almighty God, our heavenly Father, we have sinned against you and against our neighbors, in thought and word and deed, in the evil we have done and in the good we have not done, through our own deliberate fault. We are truly sorry, and repent of all our sins. For the sake of your Son Jesus Christ, who died for us, forgive us all that is past; and grant that we may serve you in newness of life to the glory of your name. Amen.

A minister or other person who is not a priest, kneeling should use this request:

Grant, we ask you, merciful Lord, to your faithful people pardon and peace, that they may be cleansed from all their sins, and serve you with a quiet mind, through Jesus Christ our Lord.

All Amen.

ZABURI 23

- 1 BWANA ndiye mchungaji wangu,
Sitapungukiwa na kitu.
 - 2 Katika malisho ya majani mabichi hunilaza,
Kando ya maji ya utulivu huniongoza.
 - 3 Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza
Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.
 - 4 Naam, nijapopita kati ya bonde la kivuli cha mauti, Sitaogopa mabaya;
Kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji.
 - 5 Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu.
Umenipaka mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika.
 - 6 Hakika wema na fadhili zitanifuata Siku zote za maisha yangu;
Nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele.
- Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu:
kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa, hata milele na milele. Amina.

WIMBO

Kuketi. Kipande kinachotoka AGANO LA KALE kisomwe.

SOMO LA KWANZA

Matendo 9:36-43

Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Matendo ya Mitume.
Na mwanafunzi mmoja alikuwako Yafa, jina lake Tabitha, tafsiri yake ni Dorkasi (yaani paa); mwanamke huyu alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa. Ikawa siku zile akaugua, akafa; wakati walipokwisha kumwosha, wakamweka ghorofani. Na kwa kuwa mji wa Lida ulikuwa karibu na Yafa, nao wanafunzi waliosikia ya kwamba Petro yuko huko, wakatuma watu wawili kwake, kumsihi na kusema, Njoo kwetu pasipo kukawia. Petro akaondoka akafuatana nao. Ali-pofika, wakampeleka juu ghorofani wajane wote wakasimama karibu naye, wakilia na kumwone-sha zile kanzu na nguo alizozishona Dorkasi wakati ule alipokuwa pamoja nao. Petro akawatoa nje wote, akapiga magoti, akaomba, kisha akaelekea yule maiti, akanena, Tabitha, inuka. Naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro akajiinua, akaketi. Akampa mkono, akamwinua; hata kisha akawaita wale watakatifu na wajane akamweka mbele yao, akiwa hai. Ikajulikana katika mji mzima wa Yafa; watu wengi wakamwamini Bwana. Basi Petro akakaa siku kadhaa huko Yafa, nyumbani mwa mtu mmoja, jina lake Simoni, mtengenezaji wa ngozi.
Hilo ndilo Neno la Bwana.
Asante kwa Mungu.

WIMBO

Kuketi. Kipande kinachotoka AGANO JIPIYA kisomwe.

SOMO LA PILI

Ufunuo 7:9-17

Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Ufunuo wa Yohana.
Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhes-abu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-kondoo. Na malaika wote walikuwa wakisimama pande zote za kile kiti cha enzi, na za

The Psalm of the Day should be read or sung. All the people read half a line after the reader.

PSALM 23

1 The Lord is my shepherd;

I shall not want.

2 He makes me lie down in green pastures;

he leads me beside still waters;

3 he restores my soul.

He leads me in right paths for his name's sake.

4 Even though I walk through the darkest valley, I fear no evil,

for you are with me; your rod and your staff, they comfort me.

5 You prepare a table before me in the presence of my enemies;

you anoint my head with oil; my cup overflows.

6 Surely goodness and mercy shall follow me all the days of my life,

and I shall dwell in the house of the Lord my whole life long.

Glory be to the Father, and to the Son, and to the Holy Spirit:

As it was in the beginning, is now, and ever shall be, world without end. Amen.

HYMN

All Sit. A passage from the OLD TESTAMENT should be read.

FIRST READING

Acts 9:36-43

Let the reader say first:

Hear the Word of the Lord as written in the Acts of the Apostles.

Now in Joppa there was a disciple whose name was Tabitha, which in Greek is Dorcas. She was devoted to good works and acts of charity. At that time she became ill and died. When they had washed her, they laid her in a room upstairs. Since Lydda was near Joppa, the disciples, who heard that Peter was there, sent two men to him with the request, "Please come to us without delay." So Peter got up and went with them; and when he arrived, they took him to the room upstairs. All the widows stood beside him, weeping and showing tunics and other clothing that Dorcas had made while she was with them. Peter put all of them outside, and then he knelt down and prayed. He turned to the body and said, "Tabitha, get up." Then she opened her eyes, and seeing Peter, she sat up. He gave her his hand and helped her up. Then calling the saints and widows, he showed her to be alive. This became known throughout Joppa, and many believed in the Lord. Meanwhile he stayed in Joppa for some time with a certain Simon, a tanner.

The Word of the Lord.

Thanks be to God.

HYMN

All Sit. A passage from the NEW TESTAMENT should be read.

SECOND READING

Revelation 7:9-17

Let the reader say first:

Hear the Word of the Lord as written in the Revelation to John.

I looked, and there was a great multitude that no one could count, from every nation, from all tribes and peoples and languages, standing before the throne and before the Lamb, robed in white, with palm branches in their hands. They cried out in a loud voice, saying, "Salvation belongs to our God who is seated on the throne, and to the Lamb!" And all the angels stood around the throne and around the elders and the four living creatures, and they fell on their

hao wazee, na za wale wenye uhai wanne, nao wakaanguka kifudifudi mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujudu Mungu, wakisema, Amina; Baraka na utukufu na hekima na shukrani na heshima na uweza na nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina. Akajibu mmoja wa wale wazee akiniambia, Je! Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? Na wametoka wapi? Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala joto iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.

Hilo ndilo Neno la Bwana.

Asante kwa Mungu.

WIMBO

HABARI NJEMA

Yohana 10:22-30

Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Injili ya Yohana Mtakatifu.

Basi huko Yerusalemu ilikuwa sikukuu ya kutabaruku; ni wakati wa baridi. Naye Yesu alikuwa akitembea hekaluni, katika ukumbi wa Sulemani. Basi Wayahudi walimzunguka, wakamwambia, Hata lini utatuhangaisha nafsi zetu? Kama wewe ndiwe Kristo, utuambie waziwazi. Yesu akawajibu, Niliwaambia, lakini ninyi hamsadiki. Kazi hizi ninazozifanya kwa jina la Baba yangu ndizo zinazonishuhudia. Lakini ninyi hamsadiki, kwa sababu hammo miongoni mwa kondoo wangu. Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu. Mimi na Baba tu mmoja.

Hilo ndilo Neno la Bwana.

Asante kwa Mungu.

WIMBO WA INJILI

KUHUBIRI

IMANI YA MITUME

Watu wasimame kuhakikisha IMANI YA MITUME

Ninamwamini Mungu, Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na dunia; Na Yesu Kristo, Mwana wake wa pekee, Bwana wetu, aliyetwaa mwili kwa tendo la Roho Mutakatifu, akazaliwa na Bikira Maria. Akateswa zamani za Pontio Pilato, akasulibiwa, akafa, akazikwa, akashuka kuzimuni mwa wafu, akafufuka katika wafu siku ya tatu, akapanda mbinguni, anakaa kwa mukono wa kuume wa Mungu, Baba Mwenyezi, ndipo atakuja tena kuhukumu wazima na wafu. Ninamwamini Roho Mutakatifu, Kanisa katolika takatifu, ushirika wa watakatifu, on-doleo la zambi, ufufuko wa mwili, na uzima wa milele. Amina.

faces before the throne and worshiped God, singing, "Amen! Blessing and glory and wisdom and thanksgiving and honor and power and might be to our God forever and ever! Amen." Then one of the elders addressed me, saying, "Who are these, robed in white, and where have they come from?" I said to him, "Sir, you are the one that knows." Then he said to me, "These are they who have come out of the great ordeal; they have washed their robes and made them white in the blood of the Lamb. For this reason they are before the throne of God, and worship him day and night within his temple, and the one who is seated on the throne will shelter them. They will hunger no more, and thirst no more; the sun will not strike them, nor any scorching heat; for the Lamb at the center of the throne will be their shepherd, and he will guide them to springs of the water of life, and God will wipe away every tear from their eyes."

The Word of the Lord.
Thanks be to God.

HYMN

GOSPEL READING

John 10:22-30

Let the reader say first:

Hear the Word of the Lord as written in the Gospel of St. John.

At that time the festival of the Dedication took place in Jerusalem. It was winter, and Jesus was walking in the temple, in the portico of Solomon. So the Jews gathered around him and said to him, "How long will you keep us in suspense? If you are the Messiah, tell us plainly." Jesus answered, "I have told you, and you do not believe. The works that I do in my Father's name testify to me; but you do not believe, because you do not belong to my sheep. My sheep hear my voice. I know them, and they follow me. I give them eternal life, and they will never perish. No one will snatch them out of my hand. What my Father has given me is greater than all else, and no one can snatch it out of the Father's hand. The Father and I are one."

The Word of the Lord.
Thanks be to God.

HYMN OF THE GOSPEL

SERMON

THE APOSTLES' CREED

All People should stand and say the APOSTLES' CREED:

I believe in God, the Father almighty, creator of heaven and earth; I believe in Jesus Christ, his only Son, our Lord. He was conceived by the power of the Holy Spirit and born of the Virgin Mary. He suffered under Pontius Pilate, was crucified, died, and was buried. He descended to the dead. On the third day he rose again. He ascended into heaven, and is seated at the right hand of the Father. He will come again to judge the living and the dead. I believe in the Holy Spirit, the holy catholic Church, the communion of saints, the forgiveness of sins the resurrection of the body, and the life everlasting. Amen.

MAOMBI

Kupiga magoti

Muhudumu Bwana utuhurumie.
Wote **Kristo utuhurumie.**
Muhudumu Bwana utuhurumie.

SALA YA BWANA

Wote

Baba yetu, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, duniani kama mbinguni. Utupe leo chakula chetu cha kila siku; utusamehe makosa yetu, kama tunavyowasamehe waliotukosea. Usitulete katika majaribu, lakini utuokoe katika uovu. Kwani kwako ufalme, uwezo na utukufu, milele na milele, Amina.

Muhudumu Ee Bwana utuonyeshe rehema yako;
Wote **Utupe sisi wokovu wako.**
Muhudumu Ee Bwana uwabariki watawala wetu;
Wote **Utusikie kwa rehema yako tukikuomba.**
Muhudumu Uwavike haki wahudumu wako;
Wote **Uwafurahishe wachaguliwa wako.**
Muhudumu Ee Bwana uwaokoe watu wako;
Wote **Uubariki uriti wako.**
Muhudumu Ee Bwana utupe salama kwa siku zetu;
Wote **Na utukufu wako uwe popote duniani.**
Muhudumu Ee Mungu, utusafishe mioyo yetu;
Wote **Na ututegemeze na Roho yako Mutakatifu.**

SALA YA SIKU

Mungu wa salama, uliyerudisha toka wafu Bwana wetu Yesu Kristo, aliye Muchungaji mukubwa wa kondoo; kwa damu ya agano la milele, utufanye sisi kuwa wakamilifu katika yote yaliyo mema, ili tutimize mapenzi yako, na ufanye ndani yetu linalokupendeza; kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

SALA KWA SALAMA

Baba Mungu, uliye mkuu wa salama na mupenda wa upatano, kukujua wewe ni uzima wa milele, kukutumikia wewe ni uhuru wa kweli. Utulinde sisi watumishi wako katika mashambulio yote ya adui zetu; ili sisi tukitumainia ulinzi wako, tusiogope nguvu ya adui wo wote; kwa uwezo wa Yesu Kristo, Bwana wetu. **Amina.**

SALA KWA NEEMA

Muhudumu na watu wanaweza kusema pamoja.

Ee Bwana, Baba yetu ya mbinguni, Mungu Mwenyezi unayeishi milele, uliyetusaidia tuone siku hii salama; utulinde leo kwa uwezo wako mkuu, tusianguke katika zambi, wala tusiingie katika hatari yo yote, lakini matendo yetu yote yaongozwe nawe, ili tuyatende siku zote yaliyo ya haki mbele yako, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

THE PRAYERS

All that are able to should kneel:

Minister Lord, have mercy upon us.

All **Christ, have mercy upon us.**

Minister Lord, have mercy upon us.

THE LORD'S PRAYER

All pray.

Our Father in heaven, hallowed be your Name, your kingdom come, your will be done, on earth as in heaven. Give us today our daily bread. Forgive us our sins as we forgive those who sin against us. Save us from the time of trial, and deliver us from evil. For the kingdom, the power, and the glory are yours, now and for ever. Amen.

Minister Show us your mercy, O Lord;

All **And grant us your salvation.**

Minister O Lord, save the State;

All **And mercifully hear us when we call upon you.**

Minister Endue your ministers with righteousness;

All **And make you chosen people joyful.**

Minister O Lord, save your people;

All **And bless your inheritance.**

Minister Give peace in our time, O Lord.

All **May your glory be everywhere in the world .**

Minister O God, make clean our hearts within us;

All **And take not your Holy Spirit from us.**

THE COLLECT OF THE DAY

God of salvation, who brought back from the dead our Lord Jesus Christ, who is the great Shepherd of the sheep; with the blood of the eternal covenant, make us perfect in all that is good, so that we may fulfill your will, and do in us what pleases you; to Jesus Christ our Lord. **Amen.**

THE COLLECT FOR PEACE

O God, who art the author of peace and lover of concord, in knowledge of whom standeth our eternal life, whose service is perfect freedom: Defend us, thy humble servants, in all assaults of our enemies; that we, surely trusting in thy defense, may not fear the power of any adversaries; through the might of Jesus Christ our Lord. **Amen.**

THE COLLECT FOR GRACE

The Minister and the people say this prayer together.

O Lord, our heavenly Father, almighty and everlasting God, who has safely brought us to the beginning of this day; defend us in the same with your mighty power; and grant that this day we fall into no sin, neither run into any kind of danger, but that all our doings may be ordered by your governance, to do always that is righteous in your sight; through Jesus Christ our Lord. **Amen.**

MAOMBI YA KANISA

Muhudumu Tuombe Kanisa na dunia na tumushukuru Mungu kwa wema wake wote.

Mwombezi huomba kwa ajili ya mahitaji ya kanisa na ya ulimwengu pasipo kuona. Muombezi anamaliza sala kwa maneno haya:

Na tunalisifu jina lako takatifu kwa watumishi wako wote wanaotoka katika uzima huu, wanaokuamini na wanaokuogopa. Tunakusihi utupe neema tufuate desturi zao nzuri, tukutane nao katika ufalme wako wa mbinguni. Utupe sisi hivi, Ee Bwana, kama tunavyoviomba kwa Yesu Kristo Mwana wako, Mwokozi wetu. **Amina.**

Maombi mengine yanaweza kusemwa.

MATANGAZO NA SADAKA

Wimbo na kupokea sadaka.

NEEMA

Watu Wote.

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapendo ya Mungu Baba, na ushirika wa Roho Mutakatifu, ukae nasi sote, milele na milele. Amina.

WIMBO YA KUTOKA

PRAYERS OF THE CHURCH

Minister Let us pray for the Church and the world and let us thank God for all his goodness.

The intercessor prays for the needs of the church and the world extemporaneously. The intercessor ends the prayer with these words:

And we praise your holy name for all your servants who have departed this life, who believe in you and who fear you. We ask you to give us the grace to follow their good example, to meet them in your heavenly kingdom. Grant this, O Lord, as we ask for it from Jesus Christ your Son, our Savior. **Amina.**

Other prayers may be said.

ANNOUNCEMENTS AND OFFERING

A song is sung during the offering.

THE GRACE

All Say

The grace of our Lord Jesus Christ, and the love of God, and the fellowship of the Holy Spirit, be with us all evermore. Amen.

RECESSIONAL HYMN

WAHUDUMU WA LITURUJIA

Muhubiri/Preacher - Bikole Mulanda

Kwaya/Choir - Aleluya Kwaya

Washemasi/Greeters & Ushers - Baya Lushiawe, Mkyombwe



602 Meander Street Phone: (325) 677-2091
Abilene, Texas 79602 Email: info@heavenlyrestabilene.org
Website: heavenlyrestabilene.org Social media: [@heavenlyrestabilene](https://www.facebook.com/heavenlyrestabilene)

CLERGY AND STAFF

The Reverend David F. Romanik, <i>Rector</i>	Luke Waters, <i>Coordinator for Youth and Young Adult Ministries</i>
The Reverend Amanda Watson, <i>Assistant Rector for Community Life</i>	Luke Teten, <i>Verger</i>
The Reverend Karen Boyd, <i>Assisting Priest</i>	Lydia Hurt, <i>Interim Office Manager</i>
The Reverend Dr. Doug Thomas, <i>Priest in Residence</i>	Brenda Fisher, <i>Interim Parish Bookkeeper</i>
The Reverend Dr. Russell Dickerson, <i>Deacon</i>	Melody Brown, <i>Website Manager</i>
Bikole Mulanda, <i>Swahili Minister</i>	Austin Hackel, <i>Communications Coordinator</i>
Thomas Pavlechko, <i>Organist and Director of Music</i>	Robert Becerra, <i>Sexton</i>
Shelly Reed, <i>Music Assistant, Choristers</i>	Brandon Martin, <i>Assistant Sexton</i>
Laura Dickson, <i>Music Assistant, Children's Choir</i>	Dorothy Guerra, <i>Housekeeper</i>
Carol Ann Weston, <i>Director of Children & Family Ministries</i>	Anne Jones, <i>Nursery Manager</i>

VESTRY AND APPOINTED OFFICERS

Kate Haney, *Senior Warden*; Harry Hurt, *Junior Warden*; Sharon Lawler, *Secretary*; David Christianson, Michael Christie, Dru Hall, Diane Stearns, Kimberly Brumley, Jay Hardaway, Norene Mansell, John Nichols, Mary Reyes, Elizabeth Niblo Wallace, *Chancellor*; and Sam Cutbirth, *Treasurer*